# Fursa ya soko la nyama itakavyonufaisha wafugaji

"Tumeleta mbegu bora kutoka Afrika Kusini inaitwa Brahman ambapo jike hufika mpaka kilo 600 ambao ni tofauti na jike la ngombe wa kienyeji ambalo hufikia hadi kilo 280 tu, ambayo ni tofauti kubwa katika uzalishaji na gharama za utunzaji..."

Na SCOLASTICA MSEWA







KIWANDA CHA TANCHOICE







"Tumeleta mbegu bora kutoka Afrika.

Scanned with CamScanner

Habari Leo, Agosti 6,2021



# Wafugaji watakiwa kuzalisha ngozi bora kupata soko imara

Na Upendo Mosha, Moshi

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai amewataka wafugaji mkoani humo kuzalisha mifugo kwa wingi na ubora ili wanufaike na uwepo wa kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi cha Karanga kilichopo katika Manispaa ya Moshi.

Kigaigai alibainisha hayo jana alipofanya ziara katika kiwanda hicho kuangalia shughuli za uzalishaji zinavyoendelea pamoja na kuzungumza na uongozi wa kiwanda.

Alisema wingi na ubora wa mazao ya ngozi katika mifugo yao utawawezesha kupata soko la uhakika katika kiwanda hicho kinachojikita katika uzalishaji wa bidhaa bora na hivyo, kuongeza pato lao, kiwanda na kuchangia ukuaji wa pato la taifa.

Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha jozi za viatu 1,000 kwa siku.

Mitambo ya uzalishaji itakapokamilika baadaye, kiwanda hicho kinalenga kuzalisha jozi za viatu 4,000 kwa siku.

"Ni vizuri sasa muanze kazi ya kutoa elimu kwa wafugaji ili wajue sasa mna kiwanda kikubwa ambacho kitanunua ngozi kutoka kwao na kuleta hapa kwa ajili ya kuchakata ili wafugaji waanze kutunza mifugo yao vizuri. Hii itakuwa ni fursa nzuri sana kwa wananchi wetu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Masoud Omary, alisema changamoto wanayokabiliana nayo kwa sasa ni upatikanaji wa ngozi zenye ubora licha ya kwamba Tanzania ina kiasi kikubwa cha ngozi.

"Soko letu ni zuri, wananchi wamepokea bidhaa zetu na tutaendelea kufanya vizuri katika masomo yetu, changamoto iliyopo sasa ni ubora wa ngozi ghafi kwa sababu hapa nchini tuna kiasi kikubwa cha ngozi, lakini haina ubora ambao unatusaidia sisi kuzalisha viatu katika ubora ambao tunaoutaka," alisema.

Aidha alisema kiwanda hicho kinatarajia kuzalisha jozi za viatu 4,000 kwa siku hapo kitakapokamilika na kusema kwa sasa kiwanda kinazalisha jozi za viatu 1,000 kwa siku.

Scanned with CamScanner